



USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



UANZISHWAJI WA MAENEO YA USIMAMIZI WA PAMOJA WA UVUVI

MAANA YA USIMAMIZI WA PAMOJA

Ni pale ambapo Shehia au vijiji zaidi ya viwili vinapokubaliana kushirikiana kusimamia eneo kwa pamoja maeneo yao ya uvuvi. Katika utaratibu huu, wadau wanakubaliana kupanga na kufanya shughuli zao kwa kushirikiana ili kuondoa changamoto ziliopo kwa ajili ya kufikia kiwango kizuri cha usimamizi endelevu.



FAIDA ZA USIMAMIZI WA PAMOJA WA MAENEO

- Kupunguza gharama
- Kudhibiti uhalifu
- Kuwa na haki ya kutumia vifaa vya usimamizi kwa kila mmoja kama vile boti
- Kurahisisha kuwakamata wahalifu na kupunguza uvuvi haramu
- Kuwa na mipango na taratibu za uendeshaji zinazolingana
- Ustawi wa rasilimali za bahari
- Ustawi wa mashirikiano ya kijamii

HATUA ZINAZOPITIWA KATIKA KUANZISHA USIMAMIZI WA PAMOJA

- Kupata idhini na makubaliano na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi pamoja na Halmashauri ya Wilaya
- Kujenga uelewa wa jamii kuhusiana na usimamizi wa pamoja kupitia mikutano mbali mbali ya Shehia
- Kukubaliana kwa Shehia au vijiji husika kupitia kamati za uvuvi za Shehia au vijiji husika
- Kuunda kamati itakayoratibu usimamizi wa pamoja wa eneo
- Kuandaa mpango wa pamoja wa usimamizi wa maeneo husika
- Kuandaa ramani ya maeneo
- Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa maeneo ya pamoja
- Kujenga uelewa wa wanajamii kuhusiana na makubaliano
- Kufanya doria ya pamoja
- Kuunganisha sheria ndogo ndogo za usimamizi




UONGOZI WA USIMAMIZI WA PAMOJA

Uongozi wa usimamizi wa eneo la pamoja unaundwa na viongozi wafuatao:

- Wajumbe wa kamati ya uratibu wa usimamizi wa pamoja
- Wajumbe watatu kutoka kila kamati ya uvuvi husika ambapo
- Sheha kutoka kila Shehia
- Diwani wa eneo husika
- Mjumbe mmoja kutoka kamati ya doria
- Mshika fedha kutoka kila kamati

Kamati hii ya uratibu itaongozwa kama ifuatavyo:

- (i) Mwenyekiti na msaidizi wake
- (ii) Katibu na msaidizi wake
- (iii) Mshika fedha



MAJUKUMU YA KAMATI YA USIMAMIZI WA PAMOJA

- Kuandaa na kuratibu mpango wa usimamizi wa pamoja
- Kuandaa na kuratibu kufanya doria za pamoja
- Kufanya mkutano mkuu mara mbili kwa mwaka utaojumuisha wajumbe wa kamati zote za uvuvi zilizokubaliana
- Kuandaa na kufuatilia mpango kazi wa pamoja na
- Kuweka mlinganisho wa sheria ndogo
- Kuratibu utaratibu wa mawasiliano